Kwako bibi

Mashauri machache kwa kumpokea bwana nyumbani

Akina mama Mubagwa Ntawiniga, mmoja kati ya tumishi wa gazeti JUA atulea hapa chini ma-ache kuhusu namna ya kumpokea bwana nyumbani sha kazi ngumu za mchana.

atika maisha ya watu niani yaonekana kuwa bibi ndiye anayemfua- bwana katika haraka- za kuongoza nyumba. yeye ndiye anayechu- a ngazi ya pili kisha ana.

maa musimokuwa bibi kama vile mti usio- va matunda.

isi wote tunafahamu wa ni bwana ndiye ayo kazi ya kutafuta za kusudi jamaa lake ishi bila uwasiwasi wote. Ndiyo maana apojielekeza kazini faa kumtunza vema na aporudi kisha kazi umu za mchana, twaomba kumpokea na kumtia katika furaha kubwa ya kuishi yeye pamoja na familia yote.

Tuelewe hapa kuwa furaha hiyo, ni msinji wa amani nyumbani.

Kusudi ya kuleta amani yafaa tufanye je?

-Tujaribu kuweka kila kitu pa nafasi yake. Sahani pamoja na vyungu viwekwe katika kabati jikoni. Tuepuke kuviweka juu ya meza barazani. Nguo zote zenyi uchafu zapashwa kubaki katika kitunga umbali mbali na zile zilizo safi.

-Yafaa pia kutunza vitu vya nyumbani. Kupanguza meza kisha kufagia ao kukoropa.

-Fanya nguvu yako ili nyumba impendeze na kumfurahisha bwana na mgeni wako.

Ukipata magumu kwa kujua kuipamba inaweza kujielekeza kunako "foyer social" ao kumfikia yule bibi ambaye aonekana mwenyi maarifa hayo kusudi aweze kukuelimisha. Usiwe na haya kwa kumuomba shauri.

-Uwe hakika kuwa bwana anapotoka kazini ni mwenyi kushikwa na njaa. Yafaa kuelewa namna ya kumvuta kwa kitovero ili apate kula bila hofu lolote.

Kwa hiyo umvute mezani. Ikiwezekana ule naye chakula kile. Usiwe sawa wale akina mama wengine wanayo tabia mbaya ya kuwatupia wabwana zao chakula mezani sawa vile wangelikipatia mbwa. Jambo hilo laweza hata kumkata bwana hamu ya kile chakula ingawa ana njaa kali.

-Bwana akifika na mgeni wake, si lazima atambue kuwa kuna shali nyumbani. Ufunge roho na uwakaribishe bila kuonya tatizo lako. Ujaribu kujibu bila makali ao mazarau.

Usionye kwa wageni kama unamhukumu bwana wako. Kwani kuna wakati anapofika nyumbani na wakuu wake ao watumishi wake wa kazi. Fujo yako yaweza kumpotezea heshima mbele ya wenzake.

-Kama ulipata magumu fulani mchana wewe na wenzako sokoni ao kazini ao pamoja na majirani, usitue hasira yako juu ya kichwa cha bwana. Umpashe jambo hilo kwa utaratibu kisha yeye kumaliza kula chakula.

Bibi mpenzi nipo hakika kuwa akajaribu kufuata mashauri hayo, wewe, bwana wako pamoja na watoto, mwaweza kuishi katika raha na kujaribu kupata jawabu juu ya matatizo inayo wakabili.

MUBAGWA NTAWINIGA

NENO LA WASOMAJI

umbe haifai kucheza na kindingi

a Mpenzi,

mi ni msomaji wako daima. Napenda leo uandikia hii mistari chache kusudi ya oa nje tabia mbaya wale wanaozoea ywa pombe ya moto ayozoea kuita hapa etu kindingi, kanya- a ao lutuku... Pombe yo ina vinyume vibaya a ginsi yatuletea ma- mu katika maisha yetu kila siku.

asema hivyo kutokana mifano miwili niliyo- onea mimi mwenyewe.

anza, nilimuona bwa- mmoja ambaye ana ma- raka makubwa katika irika moja linalojishimu akinywa pombe o bila kiasi. Punde logo alilewa na akaa- kutenda mambo yostahili. Alifikia a kukojoa katika uali yake na wale iokuwa wakimheshimu o zamani walianza uona kama mtu asiye- a na akili.

i, mwengine ambaye ni kiongozi, wali- ia mpaka kumfukuza ika kilabu kutokana ulevi wake huo wa nyanga.

e JUA, nilipoona bo hayo, nikatambua mba unapokunywa po- hiyo, unapoteza li na hauheshimiwe na watu. Hali hiyo eza hata kukusukuma ende mambo isiyo na ana mbele ya watu.

Unapokunywa pombe hiyo bila kiasi, waweza kufikia kulewa ovyo na kuharibu kazi. Pale wakuu wako wa kazi hawawezi kukuvumilia na mwisho wako ni kufukuzwa kazini ingawa siku hizi kazi ndiye baba na mama wako.

JUA mpenzi, nakukumbusha hapa tena amri za kindingi: kulala fasi ni fasi, kucheza na kuimba njiani, kusema siri za nyumbani, kutukanana na kukoseana adabu. Hapa naficha desturi nyingine mbaya za ulevi ambazo wewe peke yako wafahamu.

Hili ni shauri natolea kwa wasomaji wote wa JUA hata waandishi ambao wapendelea kunywa lutuku kama vile maji na kulewa sawa jogoo aliyekula mtama uliotumiwa kwa kutengeneza pombe ya aina ya kasigisi.

Msomaji wako
Simba Kizungu
Brigade anti-fraude
Douane de Kamanyola.

NLW: **Hivyo ni harifu kubwa kwa wale jamaa ambao wanayo tabia ya kunywa lutuku bila kiasi na kulewa sawa nzi.**

JUA

Gazeti la Kivu

Mwaka wa 12 n° 284 Tarehe 14 mpaka 20 Septemba 1985

Kiongozi : Mutiri-wa-Bashara

HABARI ZA POPOTE

Ujapani

Dada Mulumba katika mashindano ya urembo

Katika toleo lake la tarehe 31 agusti mpaka 1 septemba iliyopita gazeti Salongo linalopigwa chapa kila siku nuko Kinshasa latupasha kuwa akina dada Mureka Tete alichaguliwa huko Marekani kama vile mwanamke mwenyi urembo wa ngazi ya tatu.

Kisha mashindano hayo, dada Ntumba Mulumba naye alialikwa kujielekeza Ujapani ambako atagombea nafasi ya mbele duniani kwa urembo.

Mashindano hayo yalianzishwa huko Ujapani tangu tarehe mbili Septemba na yatamalizika mnamo tarhe 15 Septemba 1985.

Kufuatana na tangazo la wizara inayohusika na mazingira na utalii, inasemekana kuwa akina dada Mulumba Ntumba aliondoka Kinshasa siku ya mungu tarehe 1 septemba 1985 na kujielekeza Ujapani.

Wasomaji wetu wataelewa hapa kuwa akina dada Mulumba Ntumba ni mwanafunzi kunako Univasti ya huko Kinshasa ambako anajifunza mambo ya sheria.

K.H.

Michezo

"Léopards" yaondoshwa katika kombe la Afrika

Wazaliwa wa Zaïre kwa jumla na wale wapendelevu wa mchezo wa kandanda wa Jamhuri nzima ya Zaïre kwa upekee walibaki wenyi kusaga meno na kubabaika wakati jeshi lao lilipoondoshwa katika mashindano ya kugombea kombe la Afrika la mataifa. Adui si mwengine bali Moroko.

Chui wa nyika (léopards) wanaochezea majeshi ya kulipa barani Ulaya na wale wanaoshiriki katika mashindano ya hapa nyumbani hawakuweza kuwika na kuwina kunako uwanja Mobutu mtaani Kenya, mjini Lubumbashi katika jimbo la Shaba.

Wachezaji wa Zaire walifanya vyote wawezavyo kusudi ya kujipatia ushindi lakini, lah !

Wakati refari alipopiga filimbi ya mwisho kwa kumaliza pambano, Léopards na Moroko walikuwa wakianguka mabwa ya suluhu kwa suluhu (0-0).

Chui wa nyika walipewa penalty lakini Kabongo ambaye aliikunguta, hakuwahi kuisukuma katika nyavu za Moroko kwani kipa wao Zaki alizuia mpira kwa mguu wake wa kushoto.

Wasomaji wetu watakumbuka hapa kuwa katika mchezo wa mzunguko wa kwanza, chui wa nyika waliangushwa kwa goli moja kwa yayi kunako uwanja Muhamed V mjini Casablanca (Moroko).

Kufuatana na sheria ya mchezo wa kandanda, Moroko iliweza kujipatia barua ya kuingia katika fainali itakayoendeshwa huko Kairo, mji mkuu wa Misri, marsi 1986 na kuiacha chui wa nyika ikingoroma na kusaga meno.

Majeshi yafuatayo ndiyo yatakayoshiriki katika fainali ya kombe la Afrika:Moroko, Misri, Cameroun, Algeria, Zambia, Puani la pembe na Sénégal.

K.H.